BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 04 Juni, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

227. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Je, Serikali ina mpango gani wa kuzijenga ofisi za Wakuu wa Wilaya.

263. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Bado suala la kuzagaa kwa taka hapa Zanzibar ni changamoto inayoendelea kuwakabili wananchi wengi.

(a) Ni ipi mikakati ya Serikali ya kudhibiti utupaji wa taka kiholela ili kukabiliana na maradhi mbalimbali katika jamii.

(b) Ni lini Serikali italipatia Baraza la Mji Mkoani vifaa vya ukusanyaji taka kama gari ili kusaidia ukusanyaji wa taka.

(c) Je, kwa kiasi gani Serikali ipo tayari kujenga dampo maalum katika jimbo la Mkoani ili kuwa na sehemu maalum ya kutupia taka.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

355. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) wafanyakazi wa Zanzibar walikuwa wanapata haki zote za pencheni na kiinua mgongo. Hata hivyo, utaratibu huu umeendelea mpaka sasa baada ya kuja kwa ZSSF.

(a) Je, ni utaratibu upi unatumika kuwalipa kiinua mgongo na pencheni watumishi ambao wamefanyakazi katika mifumo yote miwili, wa kabla na baada ya kuanzishwa ZSSF.

(b) Je, ni utaratibu gani (kikokotoa) unaotumika kukokotoa kiinua mgongo na pensheni kwa ZSSF.

520. MHESHIMIWA ABDULLAH KAMBOTWE ABDULLAH (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

(a) Je, uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa ni upi kwa sasa.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza mapato ya ndani bila ya kutegemea sana misaada na mikopo ya nje.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

201. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Zanzibar imekuwa na historia kubwa na ya miaka mingi katika nyanja mbalimbali za harakati za kisiasa, elimu, biashara sanaa pamoja na utangamano wa jamii yake, hali iliyoipelekea kutambulika ulimwenguni kote na kupigiwa mfano katika uso wa dunia.

(a) Ni lini Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaanzisha mitaala rasmi itakayoelezea historia ya ukweli ya Zanzibar itakayokuwa ndio kielelezo cha kuwaelimisha vizazi vyetu.

(b) Ni upi mpango wa Serikali wa kuzizuia taasisi zinazotumika kuipotosha historia halisi ya Zanzibar.

**Wizara ya Afya:**

97. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na juhudi kubwa na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Nane katika kuimarisha huduma za afya, bado kuna tatizo la kutoa huduma bora kwa wananchi hasa tatizo la uzembe kwa baadhi ya wahudumu wa Vituo vya Afya nchini.

(a) Kwa kuwa jambo hili limekuwa la muda mrefu sana na linapigiwa kelele kila siku, je Serikali itakuja na mpango gani wa kudumu wa kuliondoa tatizo la uzembe kwa baadhi ya wahudumu wa afya.

(b) Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha unaomalizika, ni wahudumu wangapi wazembe wamechukuliwa hatua na hatua gani zilizochukuliwa.

(c) Je, Serikali inachukuwa hatua zipi kwa wananchi wanaoathirika na uzembe wa baadhi ya wahudumu wa afya kama vile kuwapa fidia na hata ushauri nasaha ili kuwaondolea machungu ya athari wanazopitia.

395. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwepo na taarifa kuwa madaktari waliopo chini ya Serikali wameongezewa posho ya Shilingi Laki Tano (Tsh. 500,000) katika mishahara yao wakati wauguzi na kada nyengine za afya wakikosa nyongeza hiyo licha ya mchango wao mkubwa katika utoaji huduma za afya.

(a) Ni vigezo gani vilivyotumika kuongeza posho kwa Kada ya Udaktari pekee na kuacha kada nyengine za afya.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha kuwa kuna usawa na haki katika maslahi ya watumishi wote wa Sekta ya Afya Zanzibar.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

83. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni Serikali imechukuwa hatua za dharura za kutatuwa changamoto ya umeme hasa wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Na kwa mujibu wa taarifa ya Serikali kupitia Waziri wa Wizara hii, kumeletwa meli ya kuzalisha umeme wa dharura kutoka Marekani na kuna majenereta yatawashwa.

(a) Je, kuna mafanikio yoyote yamepatikana kutokana na hatua za dharura zilizochukuliwa.

(b) Je, meli ya Marekani iliyoletwa kuzalisha umeme wa dharura, gharama za kutoa huduma hiyo ni kiasi gani na zimetoka katika bajeti ipi.

(c) Je, kwa kuwa zile ni hatua za dharura, ni lini hasa hatua za kudumu za kutatuwa changamoto ya umeme zitachukuliwa ikiwemo Zanzibar kuzalisha umeme wake yenyewe badala ya kutegemea TANESCO.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

442. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kila ifikapo mwezi wa Ramadhani na Mfunguo Tatu ya kila mwaka, watoto wetu husheherekea sikukuu hizo kwa utaratibu uliowekwa na nchi yetu.

Je, Serikali ina mpango gani ya kuwajengea kiwanja cha kudumu cha kufurahisha watoto na wananchi wa Wilaya ya Micheweni na vitongoji vyake.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

364. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Licha ya jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali za kuhakikisha Zanzibar inakuwa na miundombinu bora ya barabara, bado kuna changamoto ya ubovu wa barabara ya Mchangani Kibuleni kwenda Kijibwemtu.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuijenga barabara hiyo.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

323. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Ili kufikia malengo ya uchumi wa kidijitali, upatikanaji wa rasilimali watu wenye ujuzi wa fani ya TEHAMA ni jambo la msingi katika kuimarisha matumizi ya teknolojia na utoaji wa huduma za kisasa.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza na kuongeza wataalamu katika fani ya TEHAMA ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa kidijitali.

(b) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa kuimarisha mafunzo na elimu ya TEHAMA katika ngazi mbalimbali ili kuzalisha wataalamu wenye ujuzi unaohitajika.

(c) Serikali ina mpango gani wa kuwavutia na kuwabakiza wataalamu wa TEHAMA katika sekta za umma na binafsi ili kuimarisha utekelezaji wa ajenda ya uchumi wa kidijitali Zanzibar.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

406. MHESHIMIWA JAKU HASHIM Ayoub (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Hoteli ya Bwawani ni miongoni mwa hoteli zilizokuwa na haiba ya kipekee hapa Zanzibar kwa miaka mingi na ni moja kati ya alama zilizoachwa na Muasisi ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Mzee Abeid Amani Karume. Hata hivyo, hivi sasa hali ya hoteli hiyo inasikitisha na imekuwa kama magofu ya zamani. Pamoja na kujitokeza wawekezaji kadhaa kutaka kuwekeza, lakini maamuzi ya kuifufua tena hoteli hiyo bado hayajafanyiwa kazi na hali yake inazidi kuwa mbaya.

(a) Je, katika kuenzi jitihada za Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar Mzee Karume aliyeijenga hoteli hiyo, ni upi mpango wa Serikali wa kuinusuru hali ya Hoteli ya Bwawani.

(b) Je, kwa kuwa kuna wawekezaji waliojitokeza kuwekeza katika Hoteli ya Bwawani, ni sababu gani zimekwamisha mipango ya kuwapa wawekezaji hao.

(c) Wananchi wa Zanzibar wategemee lini Hoteli ya Bwawani kuiona inarudi kwenye haiba yake kama ilivyokuwa hapo zamani.

504. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Utamaduni wa Mzanzibari ni rasilimali muhimu inayoweza kuchangia kukuza na kuongeza thamani ya Sekta ya Utalii nchini.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza na kutumia utamaduni wa Mzanzibari katika kukuza utalii.

(b) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa kuhifadhi na kuendeleza mila, desturi na urithi wa kitamaduni ili kuvutia watalii.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashirikisha wananchi na wajasiriamali wa ndani katika kuendeleza utalii wa kitamaduni, ili kuongeza manufaa ya kiuchumi.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

174. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Pamoja na juhudi za Serikali ya Awamu ya Nane za kuinadi kauli mbiu ya Uchumii wa Buluu kwa wananchi wa Zanzibar, mpaka sasa kauli mbiu hiyo haijapokelewa ipasavyo. Hali hii ama imetokana na kukosekana kwa mipango mizuri ya Serikali au kuiamua haraka bila ya kuifanyia utafiti maalum wa kina wa kubaini athari za utekelezaji wake.

(a) Je, Serikali inachukua jitihada gani ili kuitekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya Uchumi wa Buluu.

(b) Je, Serikali imepanga utaratibu gani wa kuwashirikisha wadau wa Sekta ya Uchumi wa Buluu, ili kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kuwaondoshea riba katika mikopo iliyopo na kuwainua kiuchumi.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika kwa kipindi cha miaka mitano sasa katika kujenga madiko mapya, Unguja na Pemba.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

370. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Je, Serikali inashirikiana vipi na Taasisi za Elimu katika kuhakikisha vijana wanapata ujuzi wa kidijitali katika jimbo la Uzini.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**04 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**